# OFISI YA RAIS – TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO

SHULE YA SEKONDARI
LUKOSI,
S.L.P. 178,
**MAZOMBE.**

**Kumb. Na:** LSS/KL/F I/2020 Tarehe 18/12/2020

**JINA LA MWANAFUNZI** ...............................................

**SHULE YA MSINGI**...................................................

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUKOSI

## KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

### 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii. Shule ya sekondari Lukosi ipo katika Kijiji cha Mtandika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.

Unatakiwa kuripoti tarehe **11.01.2021** mwisho wa kuripoti tarehe **15.01.2021**.

### 2.0 SARE ZA SHULE

**a) Wavulana**

i. Suruali 2 rangi ya damu ya mzee, chini upana inchi 18 yenye mkunjo, marinda mawili juu ya mifuko ya mbele na mfuko wa nyuma usiwe na zipu.
ii. Mashati 2 meupe mikono mifupi (tetron).
iii. Viatu jozi 2 vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu.
iv. Soksi jozi 2 au zaidi rangi nyeupe.
v. Bukta moja na fulana yake, rangi ya bluu bahari au nyekundu na raba kwa ajili ya michezo.
vi. Aje na jembe 1 na mpini wake.
vii. Kwanja moja kwa ajili ya usafi.

**b) Wasichana**

i. Sketi 2 rangi ya damu ya mzee mshono wa sketi uwe na marinda ya kupanga na mfuko upande wa kushoto, mkanda wa kiunoni uwe na upana wa inchi 2 na iwe ndefu chini ya magoti.

ii. Shati (blauzi) 2 mikono mifupi (tetroni).
iii. Viatu jozi 2 rangi nyeusi vyenye kamba visivyo na kisigino kirefu.
iv. Soksi 2 au zaidi rangi nyeupe.
v. Hijab (nyeupe) kwa wasichana wa imani ya dini ya kiislamu.
vi. Bukta, singland, t-shirt rangi ya bluu bahari/ nyekundu na raba kwa ajili ya michezo.
vii. Aje na jembe 1 na mpini wake.
viii. Kwanja moja kwaajili ya usafi.

## 3.0 VIFAA VYA KUJIFUNZIA

i. Daftari kubwa – kaunta book 12 au zaidi.
ii. Kalamu, penseli, mkebe na rula.
iii. Rimu bunda 1 nyeupe (A4).
iv. Begi la kubebea daftari.
v. Kamusi moja ya kiingereza – kiswahili.

## 4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation) wa wanafunzi wa hostel.
d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza na kulinda mali za umma.

## 5.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi.
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi na kubeli.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusufi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

__________________

**MKUU WA SHULE**
**0628 060092**

## KILOLO DISTRICT COUNCIL

LUKOSI SEC SCHOOL,
P.O. Box 178,
**MAZOMBE.**

Date: 18th,December 2020.

## STUDENT'S MEDICAL FORM

To be completed by a Government Medical Officer and returned to the Head of School.

To Medical Officer
……………………………………………
……………………………………………
……………………………………………

**RE: STUDENT NAMED ……………………………………………………………………………**
**FORM …………………………………… YEAR ………………………………**

Please, examine the student mentioned above and comment on his/ her health by responding to the following items. Kindly put a tick or cross in front of either **Yes** or **No** as you find appropriate. Thank you in advance!

Do the student have problem in connection with

- Sight? **Yes/ No** if yes, state ……………………………………………
- Hearing? **Yes/ No** if yes, state ……………………………………………
- Speech? **Yes/ No** if yes, state ……………………………………………
- TB? **Yes/ No** if yes, state ……………………………………………
- Blood pressure **Yes/ No** if yes, state ……………………………………………
- Any physical disability? **Yes/ No** if yes, state ……………………………………………

Do you, therefore, recommend the said student medically fit for studentship at this school?
Yes/ No if no please state the reasons. ……………………… Signature …………………………

Name of Medical Officer ……………………………… Signature ……………………………………
Designation …………………………………… Date …………………………………… Official stamp

# OFISI YA RAIS – TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO

SHULE YA SEKONDARI
LUKOSI,
S.L.P. 178,
**MAZOMBE**

## TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili ………………………………………………………………………………
   tarehe ya kuzaliwa ……………………………………… (taja mwezi na mwaka).
2. Kabila ……………………………………………… Taifa ………………………………
3. Dini na dhehebu ………………………………………………………………………
4. Jina la Baba ……………………………………………………………………………
5. Anwani ya Baba/ Mlezi ……………………………………………………………
6. Kazi ya Baba/ Mlezi …………………………………………………………………
7. Jina la mama …………………………………… kazi yake ……………………………
8. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana ………………………………………
9. Jina na anwani ya mlezi wako au mzazi …………………………………………
10. Je, wazazi wako wote ni hai? ……………………………………………………
11. Kamwe sitajihusisha na migomo, kufanya fuko wala sitajihusisha katika makosa ya jinai.
12. Nathibitisha kuwa habari zote nilizozitoa hapoj uu ni za kweli na sahihi.

Saini ya Mwanafunzi ………………………………… Tarehe …………………………

Saini ya Mzazi/ Mlezi ………………………………… Tarehe …………………………

## SEHEMU YA MZAZI/ MLEZI

Mimi ……………………………………………………… ninakubali mtoto wangu ……………………………………………………… kuingia Shule ya Sekondari Lukosi kidato cha kwanza mwaka ……………………… ninaahidi kumpatia mahitaji yote muhimu kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule

(Joining Instructions). Ninakuhakikishia nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanafunzi anatekelezwa wajibu wake kwa shule na Taifa.

Anuani yangu ya kudumi ni:-

…………………………………………………

…………………………………………………

…………………………………………………

Iwapo nitapata uhamisho au kubadilisha kazi ni lazima nitajulisha shule kwa maandishi yaliyothibitishwa na Mkuu wangu wa Idara au Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata na Ofisi ya Serikali ya Kijiji.

Ndugu watatu wa karibu wanaoweza kumtembelea Mwanafunzi huyu shuleni ni wafuatao:-

1. ………………………………………………………………………………
2. ………………………………………………………………………………
3. ………………………………………………………………………………

**Saini** ……………………………… **Tarehe** ……………………

**Jaza fomu hii na kuirudisha shuleni**

---

**MKUU WA SHULE**